# Nachingwea: Kitovu fursa za biashara na uwekezaji

Na Selemani Nzaro, Lindi

**WILAYA ya Nachingwea ni miongoni mwa wilaya kongwe katika Mkoa wa Lindi. Ni miongoni mwa wilaya tano zinazounda Mkoa wa Lindi. Nyingine ni Lindi, Kilwa, Liwale na Ruangwa.**

Wilaya hii inapakana na Wilaya za Ruangwa kwa upande wa Kaskazini Mashariki, Masasi Mkoani Mtwara kwa upande wa Kusini Mashariki, Tunduru mkoani Ruvuma kwa upande wa Kusini Magharibi na Liwale kwa upande wa Kaskazini Magharibi.

## IDADI YA WATU

WILAYA ya Nachingwea ina ukubwa wa kilomita za mraba 7070 zenye tarafa tano ambazo ni Nambambo, Ruponda, Lionja, Naipanga na Kilimarondo. Wilaya hii ina jumla ya kata 36, vijiji 127, vitongoji 527 vyenye idadi ya watu wapatao 178, 464 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.

Wilaya ina mamlaka ya Mji Mdogo iliyoanzishwa mwaka 2009 ambayo ina kata tatu kati ya 36 za wilaya nzima. Uchumi wa wilaya kwa kiasi kikubwa unategemea kilimo kwa zaidi ya asilimia 80.

## SEKTA YA AFYA

Sekta ya afya imeboreshwa kwa kiasi kikubwa na inazidi kuimarika kutokana na ukarabati wa hospitali ambayo ilikuwa chakavu. Wilaya ina Hospitali ya Wilaya. Wilayah ii in hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, zahanati za vijiji na vituo vya afya.

Wilaya ya Nachingwea ina Hospitali tatu, vituo vya afya viwili na Zahanati 32. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha Afya Kilimarondo na Hospitali ya Wilaya . Ukarabati huu utaboresha upatikanaji wa huduma za Afya.

## SEKTA YA ELIMU


Nachingwea ina Shule za awali, msingi na Sekondari na vyuo. Sekta hii inahitaji uwekezaji mkubwa kwa kuwa bado shule zilizopo na miundombinu yake haitoshi kukidhi hitaji la elimu kutokana na idadi ya watu.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea Ahmad Makoroganya.




Halmashauri ya Nachingwea inawaalika wananchi na wawekezaji katika ujenzi wa Shule za awali, msingi na Sekondari ili kukidhi mahitaji ya wakazi wa wilaya hiyo kwa kutoa elimu bora zaidi.

Mkoa wa Lindi una Chuo cha Ualimu kimoja tu ambacho kipo katika Wilaya ya Nachingwea. Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nachingwea, Geofrey Nnauye, halmashauri imetenga eneo la uwekezaji ambapo mwekezaji anaweza kujenga shule za awali, msingi na sekondari.

## SEKTA YA KILIMO

Tangu enzi za ukoloni, Wilaya ya Nachingwea imekuwa ikijipambanua kama sehemu yenye ardhi nzuri ya kilimo. Wakoloni waliitumia fursa hiyo kwa kuanzisha mashamba ya karanga yaliyofahamika kwa namba zaidi kuanzia Shamba Namba 1 hadi 17 (Farm 1-17).

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nachingwea, Ahmad Makoroganya anasema ukiondoa Mamlaka ya Mji Mdogo ambayo imeundwa na kata tatu, kata nyingine 33 zinategemea kilimo kama shughuli kuu za uchumi.

"Hii inaonyesha ni kiasi gani Nachingwea inaategemea kilimo kwa sababu Wilaya yote ina kata 36 lakini ukiondoa kata tatu za Mamlaka ya Mji Mdogo zinabaki kata 33 ambazo wananchi wake njia kuu ya uchumi ni kilimo," anasema Makoroganya.

Wilaya ya Nachingwea inajishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara pamoja na mazao ya chakula. Mazao ya biashara ni kama vile korosho, ufuta na alizeti. Kwa upande wa mazao ya chakula ni kama vile mahindi, mihogo, mbaazi, karanga, mpunga na kunde.

Wilaya hii inaendesha kilimo cha aina mbili, kwanza ni kilimo cha msimu wa mvua yaani vuli na masika na kilimo cha pili ni kilimo cha umwagiliaji kupitia mabonde oevu yanayotiririsha maji mwaka mzima bila kukauka.

Asilimia kubwa ya wananchi wa Nachingwea wanategemea aina ya kwanza ya kilimo ambacho ni kilimo cha msimu kwa maana ya kutegemea mvua. Baadhi ya sehemu ndio hutegemea kilimo cha umwagiliaji kwa maana baada ya msimu wa mvua kupita wananchi wanaendelea na kilimo cha umwagiliaji.

Baadhi ya mabonde oevu

>>

> Wilaya ya Nachingwea ina mabonde makubwa ambayo ni fursa za uwekezaji ambazo wawekezaji wanaweza wakazichangamkia na kuufanya mkoa wa Lindi kuwa mkoa wa kiuwekezaji kutokana na kujaa fursa lukuki kuanzia katika kilimo, bahari, usafiri wa anga, shule, hoteli na viwanda.
>
> - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nachingwea, Ahmed Makoroganya

**17**

Idadi ya mashamba makubwa yenye ardhi nzuri ya kilimo ambayo wakoloni waliyatumia kama fursa kwa kulima karanga.



# Nachingwea: Kitovu fursa za biashara na uwekezaji






**Ujenzi wa kiwanja wa ndege Nachingwea ukiendelea. Picha ndogo ni jengo la ofisi za Uwanja huo.** Picha na Fadhili Akida

yanayosaidia katika kilimo cha umwagiliaji ni bonde la Marambo, chiola, Ruponda, Mandawa na Lionja yote hayo yakiwa na maji wakati wote wa mwaka.

Mabonde mengine ambayo yanamhakikishia mwekezaji katika sekta ya kilimo kuwa atapata mavuno ya kutosha kutokana na kuwa na maji muda wote na ardhi yenye rutuba ni kama vile bonde la Mnero-Ngongo, Mnero-Miembeni, Majonanga, Kiegei, na Kilimarondo.

Mabonde yote hayo ni fursa za uwekezaji ambazo wawekezaji wanaweza wakazichangamkia na kuufanya mkoa wa Lindi kuwa mkoa wa kiuwekezaji kutokana na kujaa fursa lukuki kuanzia katika kilimo, bahari, usafiri wa anga, shule, hoteli na viwanda.

Pia, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea imetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo kama vile Kiegei, Matekwe, Mutua, Ngunichile na Namapwia. Hayo ni baadhi ya maeneo ambayo wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza.

## SEKTA YA VIWANDA

Sekta hii ni muhimu sana katika maendeleo ya Wilaya ya Nachingwea. Hii ndiyo sababu Halmashauri ya Wilaya hiyo imetenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda mbalimbali vikiwemo vya kuchakata mazao ya kilimo, kuchakata madini na mazao ya bahari.

Baadhi ya maeneo ambayo Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea imetenga ni pamoja na Bondeni Road, Stesheni, Nangowe na Songambele. Maeneo haya yatakuwa himaya ya viwanda kwa kuwa bidhaa zote zitakazohitajika zinazalishwa kwa wingi hivyo kuongeza fursa za ajira kwa wananchi wa Nachingwea.

Eneo hili lililotengwa kwa ajili ya viwanda na uwekezaji mwingine kama masoko, shule na viwanda vya nyama na korosho lina ukubwa wa hekta 114. Hili ni eneo ambalo likiwekezwa litaleta manufaa makubwa kwa wananchi wa Nachingwea na Mkoa mzima wa Lindi.

## SEKTA YA MIFUGO

Wilaya ya Nachingwea ina mifugo ya aina mbalimbali wakiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, na ufugaji wa kuku. Kutokana na mchango mkubwa wa mapato unaotokana na sekta ya mifugo, Halmashauri ya Nachingwea imeamua kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa mifugo.

Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji yana ukubwa wa hekta 61,000 ambayo wawekezaji wanaweza kuyatumia kuwekeza mifugo kwa sababu ni sehemu inayokidhi vigezo vya ufugaji.

Maeneo hayo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo na ufugaji ni Matekwe na Mtua mahsusi kwa wawekezaji wa mifugo ndani ya Wilaya ya Nachingwea.



**114**

Idadi ya hekta ambazo Halmashauri ya wilaya ya Nachingwea imetenga kwa ajili ya wawekezaji wa aina mbali kama Viwanda, shule, masoko n.k.




## SEKTA YA MADINI

Nachingwea imebahatika kuwa moja ya wilaya nchini ambazo zina utajiri wa madini. Madini yanayopatikana katika wilaya hii ni pamoja na Nikel, Dhahabu na Vito. Rasimimali hii ipo katika kata za Nditi na Marambo.

Maeneo mengine ni pamoja na Ruponda, Chiola, Namapwia, Mbwemkuru, Naipingo, Mtepeche, Nammanga na Namatula.

Madini mengine yanayozalishwa katika maeneo hayo ni granite, kokoto, chuma na madini ujenzi.

Sekta ya madini inahitaji wawekezaji wa kutosha. Waliopo sasa ni wawekezaji wadogo wadogo wenye vifaa duni.

## SEKTA YA UTALII

Wilaya ya Nachingwea ina vivutio vingi vya utalii kama mlima Ilulu ambao umekuwa nembo ya wilaya.

Mlima huo wenye urefu wa mita 393 kutoka katika usawa wa bahari ni kivutio kikubwa cha utalii kutokana na historia yake. Mlima Ilulu ulipewa jina hilo baada ya ushindi wa vita waliopata kabila kuu katika wilaya hii la Wamwera dhidi ya Wangoni.

Ushindi ulipatikana baada ya askari wa Kimwera kupanda juu ya mlima huo na kuweka mtego wa mawe makubwa mengi. Baada ya Wangoni kufika katika eneo hilo Wamwera waliporomosha mawe hayo na kuwaponda Wangoni na kuwamaliza.

Baada ya ushindi, kiongozi wa Wamwera aliwatangazia wananchi wake ushindi na wanawake kupiga vigelegele ambavyo vilitoa sauti inayoshabihiana na neno …lulu.. ndipo ukaitwa Mlima Ilulu kwa maana ya 'mlima wa ushindi'.

Pia kuna kaburi la Chifu wa Wamwera aliyeongoza vita dhidi ya uvamizi wa

>>




# Nachingwea: Kitovu fursa za biashara na uwekezaji

Wangoni na hatimaye kutangaza ushindi baada ya kutumia mbinu ya kusukuma mawe kutoka mlimani na kuwaangamiza maadui wote. Kaburi hilo hutumika kama sehemu ya maombi na tambiko kwa jamii za Kimwera.

**Kaburi la mbwa**

Kuna kaburi la mbwa wa kizungu aliyekufa mwaka 1950 na kuzikwa wilayani Nachingwea. Mbwa huyo alifundishwa kufanya kazi za mwanadamu ambapo alikuwa akitumwa katika sehemu mbalimbali na kutekeleza amri ya bosi wake.

Kwa mujibu wa historia ya mbwa huyo, alianzia maisha yake katika mataifa ya Asia nchini Malaysia katika visiwa vya Sumatra wakati wa vita ya pili ya dunia alifika maeneo mbalimbali katika mataifa ya China, Misri, India hadi katika mataifa ya Afrika Mashariki.

**Kambi ya wapigania uhuru ya Farm 17**

Kivutio kingine katika



Nachingwea ina hifadhi nyingi za misitu ambayo ina fursa kwa wawekezaji wa mazao ya misitu



**274.3**

Idadi ya hekta za eneo la kiwanja cha ndege cha Nachingwea


Wilaya ya Nachingwea ni kuwepo kwa kambi maarufu ya wapigania uhuru wa Msumbiji ya Farm 17.

Kambi hii iliongozwa na Rais wa Kwanza wa Msumbiji, Hayati Samora Machel kati ya mwaka 1963 hadi mwaka 1975, mwaka ambao nchi hiyo ilijitangazia uhuru wake.

Kuonesha umuhimu wa kambi hiyo, Msumbiji imeendelea kuenzi wilaya ya Nachingwea kama kitovu cha Harakati za Ukombozi wake ambapo ilijenga Chuo Kikuu nchini humo na kukiita Chuo Kikuu cha Nachingwea.

Pia, Balozi wa Msumbiji nchini Tanzania amekuwa akifanya ziara za mara kwa mara katika eneo hilo ikiwa ni ishara ya kuenzi na kuonesha umuhimu wa eneo hilo katika historia ya Msumbiji na Tanzania kwa ujumla.

Baadhi ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini Msumbiji na Zimbabwe wamekuwa wakitembelea eneo hilo kujionea kitovu cha harakati za ukombozi wa mataifa ya Afrika hali ambayo inazidi kuonesha umuhimu wa eneo hilo kwa vizazi vya sasa na vijavyo.



Nachingwea imebahatika kuwa moja ya wilaya nchini ambazo zina utajiri wa madini. Madini yanayopatikana katika wilaya hii ni pamoja na Nikel, Dhahabu na Vito. Rasimimali hii ipo katika kata za Nditi na Marambo...



Kutokana na historia yake, Wilaya ina vivutio vingi vya utalii ikiwa ni pamoja na mlima wa Ilulu, kaburi la Chifu wa Wamwera, kaburi la mbwa wa kizungu,

**Kiwanja cha ndege cha Nachingwea**

Kiwanja cha Ndege cha Nachingwea ni kikongwe na kina historia kubwa iliyoanzia wakati wa ukoloni wa Waingereza. Kiwanja hicho kilijengwa na walowezi wa Kingereza waliokuwa wakishughulika na kilimo cha karanga mwaka 1947.

Baada ya uhuru wa Tanganyika chini ya uongozi wa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, serikali ilikichukua kiwanja kwa ajili ya safari za ndege za abiria na za kijeshi hususani wakati wa harakati za ukombozi wa bara la Afrika.

Ni kiwanja ambacho kilitumika katika shughuli za ukombozi wa baadhi ya nchi za Kusini mwa Bara la Afrika kama vile Msumbiji, Zimbabwe, Angola, Namibia, na Afrika Kusini.

Kiwanja kina ukubwa wa hekta 274.3 lakini sehemu kubwa ya eneo hilo la kiwanja lipo mikononi mwa wananchi na taratibu za kuwalipa fidia zinaendelea. Askari wengi waliohusika na ukombozi wa nchi hizo walikuwa na maeneo yao ya kuishi kuzunguka kiwanja hicho.

Baada ya maandalizi ya vita kwa maana ya kuwaandaa askari watakaokwenda vitani wakati wa harakati za ukombozi, walitumia ndege kwenda vitani katika nchi hizo na ndege ilikuwa ikiruka kutoka katika kiwanja hicho.

Kiwanja hicho kina njia moja ya kurukia na kutua kwa ndege na kina urefu wa mita 1,793 (takribani kilomita 1.8) yenye majina ya 14 kwa upande wa Kaskazini na 32 kwa upande wa Kusini wakati ndege inapokuja kutua.

Meneja Msaidizi wa Kiwanja hicho, Johnston Ngatora ambaye pia ni mwegesha ndege mwandamizi anasema kiwanja hicho kipo katika matengenezo ya kiwango cha changarawe hivyo kwa sasa kimefungwa kupisha kazi hiyo. Kiwanja kina majengo mawili yanayotumika kama utawala pamoja na mahali pa kupumzika abiria kabla ya kuondoka na jengo la pili ni la zimamoto.

Kwa kuwa madhumuni ya kiwanja yalikuwa ni kutoa huduma ya kusafirisha bidhaa za mazao wakati waukoloni na usafirishaji wa askari wakati wa kupigania uhuru, bado kiwanja kimezungukwa na makazi ya watu hali inayofanya uendeshaji wa kiwanja kuwa na changamoto.

Baada ya ukarabati huo kukamilika kiwanja hicho kitakuwa na uwezo wa kupokea ndege zenye ukubwa wa kati zinazobeba abiria 70 hadi 75 kama vile Bombardier zinazomilikiwa na Shirika la Ndege (ATCL) na nyingine ndogondogo.

**MISITU YA ASILI**

Wilaya ya Nachingwea ina hifadhi nyingi za misitu ambayo inamilikiwa na halmashauri na mingine inamilikiwa na serikali za vijiji. Misitu hii ina fursa nyingi kwa wawekezaji mfano mwekezaji wa mazao ya misitu kama mbao.

Misitu hii ina miti mbalimbali ambayo haijaguswa yapata miaka zaidi ya 50 hivyo inaweza kutoa mbao ngumu nzuri zinazoweza kuleta ushindani katika soko la mbao duniani.

Mbali na mbao pia misitu hiyo inaruhusu uvunaji wa magogo ambayo yanapatikana ya kila aina na yanatoka katika miti yenye umri tofauti.

Hii ni fursa kubwa kwa wawekezaji wa mazao ya misitu kuitumia kuweza kukjenga kiwanda cha mazao ya misitu ili kufanya uvunaji wa misitu kuwa mzuriusioharibu mazingira.

Misitu hiyo pia inaruhusu kufanya uwekezaji wa kilimo cha nyuki na kupata asali nzuri kutokana na misitu hiyo kuwa na mqua mbalimbali na vijito visivyokauka mwaka hadi mwaka ■



**Kaburi la mbwa ni moja ya vivutio vya utalii wilayani Nachingwea, mkoani Lindi. Mbwa huyo aliyeitwa Judy alizaliwa mwaka 1936 huko Shaghai, China kabla ya kutumiwa na wanajeshi wa Uingereza katika Vita vya Pili vya Dunia (1939-1945). Aliletwa Tanganyika (sasa Tanzania) na mmoja wa wanajeshi wastaafu wa Uingereza aliyekuja nchini kwa ajili ya mradi wa karanga Nachingwea. Mbwa huyo aliyekuwa na cheo kikubwa cha kijeshi katika Jeshi la Uingereza alikufa mwaka 1950 hapa Nachingwea. Alikufa na kujengewa kaburi na Waingereza kama kumbukumbu kwa mchango wake mkubwa katika vita hiyo.** Picha na Fadhil Akida